MAKONGORO HIGH SCHOOL

P.O. BOX 492, BUNDA.

Mawasiliano:
Mkuu wa shule: 0756 321 224, 0785 321 224, 0629 067 377,
Makamu mkuu wa shule: 0757 957 874; 0623 107 155

KUMB.NA.MAKSS/STF/F.5/J.I/2021 19/05/2021.

MWANAFUNZI_____
S.L.P. _____
_____

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAKONGORO KIDATO CHA TANO MWAKA 2021/2022</u>

1:0 Ninafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha **TANO** katika shule hii Julai 2021.Hongera sana.

Shule ya Sekondari Makongoro ni ya bweni kwa kidato cha **Tano** na **Sita**. Iko umbali wa***Km 2½*** Mashariki mwa mji mdogo wa Nyamuswa,kandokando ya barabara kuu iendayo Mugumu-Serengeti.Shule hii iko umbali wa***Km 27*** kutoka stendi kuu ya mabasi ya wilaya ya Bunda, Mkoa wa Mara.Ufikapo Bunda stendi kuu ya mabasi panda magari yanayokwenda Mugumu wilaya ya Serengeti ukifika Nyamuswa mweleze kondakta akushushe kwenye geti la shule ya sekondari Makongoro.

Kwa wanaotokea Arusha wanaweza wakashuka shuleni au stendi ya nyamswa na kuchukua pikipiki kwa gharama ya elfu moja tu (1000) hadi shuleni.

Tarehe ya kufungua shule 05/07/2021 Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **05/07/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni siku moja kabla ya tarehe ya kufungua shule.** Ofisi ya Makamu Mkuu wa shule itakuwa wazi kwa mapokezi na usajili ukiwa na:

i. "Pay in Slip" mbili zinazoonesha malipo uliyolipia Benki
ii. Kivuli cha cheti cha kuzaliwa kinachotolewa na Serikali.
iii. Kivuli cha matokeo ya mtihani wa kidato channe *(Result Slip)*
iv. Vifaa ulivyoandikiwa katika fomu hii,na fomu tatu zilizo ambatanishwa na kujazwa kwa usahihi ***(fomu iliyojazwa na daktari, fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi, ahadi ya mzazi na fomu ya kukubali masharti ya shule.)***

2:0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

2:1 SARE YA SHULE:

(a) ***Kwa Wavulana*:**
Ni suruali 02 nyeusi zenye marinda mawili na mifuko mitatu; miwili pembeni na mmoja nyuma. Suruali isiwe modo na upana wa suruali usipungue inchi 16. Mkanda wa ngozi rangi nyeusi

(b) ***Kwa Wasichana:***
Ni sketi 02 nyeusi zenye marinda, mkanda wa sketi (belti ya kiuno) usizidi inchi 1½ au sm 4. Sketi ziwe ndefu zinazogusa kiatu.

NB: Kumbuka kushona kitambaa kizito cha suti na sio kitambaa cha sukari sukari. Mwanafunzi haruhusiwi kusuka kuwa na ndevu na kunyoa mitindo.

Kwa wasichana na Wavulana:

- Shati 02 nyeupe zenye mikono mirefu, Tai nyeusi, urefu usivuke mkanda wa suruali au sketi, upana sm 7½ na iwe na kibanio.
- Soksi ndefu nyeupe jozi 02, zisiwe na urembo kwa wasichana.
- Soksi ndefu nyeusi jozi 02, zisiwe na urembo kwa wavulana.
- Viatu vyeusi vya kamba vyenye kufunika miguu viwe na kisigino kifupi na visipige kelele wakati wa kutembea kwenye sakafu.
- Sweta rangi ya bluu aina ‘v’shingo ya kuvaa wakati wa baridi.

(c) Kwa waislam wanatakiwa kuwa na hijabu rangi mbili (2) Rangi nyeupe na rangi ya bluu.

(d) **Sare ya Michezo**:

- ***Kwa wavulana*** ni ‘Track suit’ ya bluu, jezi ya rangi ya bluu na viatu vya raba nyeusi

- ***Kwa wasichana*** ni 'Track suit' ya bluu, 'T-shirt' kijani, sketi ya kaki na viatu vya raba nyeusi

(e) **Sare ya kazi**:

- 'T-shirt' 02 za bluu zenye nembo ya shule(zinapatikana shuleni kwa bei ya Tshs. 12000/=@ zina collar, Suruali 02 za kaki kwa wavulana zenye upana usiopungua inchi 16 na Gauni 02 mshono wa solo kitambaa cha kunguru ya bluu kwa wasichana kwa urefu wa kugusa viatu (aje nazo.)

NB: Mwanafunzi wa shule hii hapaswi kuja na nguo nyingine yoyote,tofauti na hizo zilizoelekezwa. Nguo za nyumbani hazitakiwi kabisa pamoja na vitu vya urembo.

2:2 ADA NA MICHANGO YA SHULE:

A: Ada ya shule kwa mwaka ni Tshs. **70,000/=** au Tshs. **35,000/=** kwa muhula. Fedha hizo zilipwe katika akaunti ya shule **Na. 30101200050** Jina la akaunti ni**RECCURENTACCOUNT MAKONGORO SECONDARY SCHOOL** Benki ya **NMB**. Akaunti hii ni kwa **AJILI YA KARO TU.**

B: **Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni**:-

i.) Tsh. 5,000/= kwa ajili ya tahadhari **(Hazirudishwi)**
ii.) Tsh. 6,000/= kwa ajili ya picha na kitambulisho
iii.) Tsh. 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
iv.) Tsh. 30,000/= kwa ajili ya walinzi, wapishi na vibarua wengine
v.) Tsh. 2,000/= Nembo ya shule
vi.) Tsh. 2,000/= Jalada (File cover)
vii.) Tsh. 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza Tsh. 5,000/= na Bima ya Afya Tsh. 5,000/=
viii.) Tsh. 16,000/=Umeme na maji
ix.) Tsh. 20,000/= kwa ajili ya Taaluma
x.) Tsh. 24000/= kwa ajili ya T-Shirt mbili (2)

Angalizo: Jumla ya ada na michango kwa wanafunzi wa Bweni ni Tsh. 200,000/=

Fedha yote ya michango ilipwe Benki ya **NMB** kwenye akaunti ya shule **Na.30101200051** Jina la akaunti ni: **DEVELOPMENT ACCOUNT MAKONGORO SECONDARY SCHOOL.**

NB: HATUPOKEI PESA TASLIMU. TAFADHALI LIPIA BENKI.

2:3 Vifaa vya kazi:

- Fyekeo kwa wasichana.
- Ndoo mbili za lita 20 kwa ajili ya kuogea na kufulia (kwa ajili ya mwanafunzi).
- Reki yenye mpini wa chuma kwa wavula .
- 'Squeezer rubber' moja, Soft Bloom moja Kwa wote na Fagio aina ya chelewa kwa wote.

2:4<u>Vifaa vya kutumia darasani na wakati wa mitihani</u>

- Rimu 02 'Double A'(kwa muhula mmoja).
- 'Counter Book' zisizopungua 10
- 'Mathematical Set' 01
- Rula ndefu 01
- Kalamu blue au nyeusi za kutosha
- 'Scientific Calculator' 01 (kwa masomo ya sayansi)
- Vitabu vya masomo kulingana na tahasusi yake **NI LAZIMA NA VITAKAGULIWA ni mali ya mwanafunzi.**

2:5<u>Vifaa binafsi vya kutumia bwenini:</u>

- Godoro moja la 'sponge' '2½' x 6'
- Chandarua
- Galoni ya lita 5 kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa
- Vyombo vya chakula(Sahani, bakuli kikombe)
- 'Toilet paper' za kutosha (kwa matumizi yake binafsi)
- Shuka 02 mpya *(rangi ya bluu)*
- Ndala/kanda mbili
- Taulo/khanga doti moja kwa wasichana
- Mto na foronya*(rangi ya bluu)*
- **Ni vizuri aje na sanduku la mbao/bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake.**
- Solata kwa tahadhari kama umeme ukikatika.

NB. Kwa wale wanafunzi wanye masomo ya Biology wanatakiwa waje na:-

- ✓ **Dissection kit** – Kwaajiri ya upasuaji wa wanyama wadogowadogo katika maabara
- ✓ **Dissection Tray** – kwa ajili ya kuwekea mnyama anayepasuliwa wakati zoezi la upasuaji likiendelea.
- ✓ **Laboratory coat** – Kwa ajili ya kuvaa wakati wa mazoezi ya maabara ya kuzuia madhara ya kemikali (pia wanafunzi wanaosoma somo la chemistry waje na labcoat).
- ✓ **Vitabu vya ziada angalau viwili Kwa somo la biology Ili kurejea baada ya vipindi vya darasani.**

3:0 **<u>SHERIA, KANUNI NA TARATIBU MUHIMU ZA SHULE HII:</u>**

3:1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Hivyo ni muhimu kwako kumkumbusha mwanao ajue umuhimu wa nafasi hii. Ni ukweli usiopingika kwamba malezi ya wanafunzi kitaaluma kiroho na kimwili yanategemea ushirikiano kati ya walimu na wazazi.

Hivyo huna budi kumkumbusha mwanao ajue fika kwamba shuleni mahala pa kupata **Elimu** na sio mahali pa kufanya starehe na vioja. Ukosefu wa mawasiliano kati ya pande mbili katika kumuendeleza mwanafunzi kitaaluma daima huzaa wahitimu wasio na ELIMU/UJUZI. Uongozi wa shule umeona ni vizuri kuwashirikisha wazazi katika malezi ya watoto wao hasa katika kuelewa sheria, kanuni na taratibu mbalimbali za jumuiya ya shule ya sekondari Makongoro. Hivyo hapa nakuletea sheria za shule

uzisome na kuzielewa.Aidha mwanao inambidi kuzisoma na kukiri mbele yako kuwa yupo tayari kuzitekeleza.

Mwisho, baada ya kusoma wewe mzazi/mlezi unaombwa kuweka jina na sahihi pamoja na mtoto wako aweke jina na sahihi akiahidi kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na atapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu

(c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule

(f) Kutunza mali binafsi, ya mtu mwingine na mali ya umma

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

(i) Kila mwanafunzi lazima ahudhurie 'Pared Ground' kila siku asubuhi na jioni. Mwanafunzi asiyehudhuria sehemu hizo atahesabika mtoro na ataadhibiwa.

Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu awapo shuleni mzazi/mlezi anatakiwa kutumia simu namba: 0757 957 874 ya Makamu mkuu wa shule au 0743 889 553 ya patron (Kwa wanafunzi wa kiume) na 0762 310678 (Kwa wanafunzi wa kike).

- **ADHABU:**
  Mwanafunzi atakayekiuka utaratibu huu atasimamishwa masomo *(suspension)* endapo atarudia atafukuzwa shule kabisa.

- **MASOMO:**
  - **i.** Mwanafunzi anatakiwa kusoma masomo yote kama alivyopangiwa na Wizara na ikiwa hatahudhuria **kipindi hata kimoja** bila sababu ya msingi **ataadhibiwa vikali au kufukuzwa shule mara moja.**
  - ii. Lugha rasmi ya shule ni kiingereza hivyo mwanafunzi anatakiwa kuitumia lugha hii katika mawasiliano baina yake na walimu pia na wanafunzi wenzake.

- **MIPAKA:**
  - i. Mwanafunzi anapofika shuleni haruhusiwi kwenda nje ya shule bila ruhusa ya MKUU WA SHULE.
  - **ii.** Ni marufuku mwanafunzi kutembelea nyumba za walimu/wafanyakazi au kutoka nje ya shule bila ruhusa maalumu ya maandishi toka kwa **Mkuu wa Shule.**

iii. Mwanafunzi atatoka nje ya shule kwa kutumia fomu maalumu iliyotolewa na MKUU WA SHULE
iv. Mwanafunzi atakayevunja sheria hii akaenda nje ya shule bila ruhusa adhabu yake ni **KUFUKUZWA SHULE.**

- **MAVAZI:**
  Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule muda wote akiwa darasani pia haruhusiwi kujipamba au kumiliki urembo wa aina yoyote.

3:1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE:

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile; uvutaji sigara, bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
5. Kupigana au kupiga au kutukana mwalimu, mfanyakazi au kiranja.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kutembelea majumba ya starehe (kama vile Baa,club n.k)
10. Kupata au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza fujo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu wengine
13. Kukataa adhabu kwa makusudi uliyopewa na mkuu wa shule, mwalimu au kiranja
14. Mwanafunzi kuwa na **SIMU** ya mkononi shuleni au kumiliki laini ya simu ama kifaa chochote kile kinachohusiana na simu.
15. Kutoroka shuleni.
16. Udanganyifu katika mitihani.
17. Kukwepa kufanya majaribio ya kila mwezi na mitihani yote.
18. Kutohudhuria masomo zaidi ya siku 90 bila taarifa au utoro
19. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua.
20. **Kuchelewa kuripoti shuleni bila taarifa yoyote shuleni.**
21. **Kupiga kelele au mayowe darasani bila sababu za msingi kama ugonjwa.**
22. **Kutega au kutoshiriki kazi mbalimbali shuleni kam vile usafi bwenini na mahali kwingineko.**

4:0 <u>MAMBO MENGINE MUHIMU:</u>

- **Shule ina mihula 02 ya masomo na kila muhula unapokwisha shule hufungwa, hivyo kwa kila mzazi/mlezi anatakiwa kumtumia mwanae nauli ya kurudi nyumbani kwa ajili ya mapumziko. Shule haitaruhusu mwanafunzi kubaki shuleni wakati wa likizo ndefu.**

- **Shule haina utaratibu wa chakula maalumu (Special Diet) kwa mwanafunzi mmoja mmoja tofauti na kile kinachoandaliwa na shule kwa ajili ya wanafunzi wote.**

- 'Medical Examination Form' ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

- Fomu za Maelezo binafsi ya Mwanafunzi

- Fomu ya Mzazi ya kukiri,kukubaliana na sheria, Kanuni, kulipia ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5:0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Tumia nafasi hii muhimu ambayo Taifa limekupa upendeleo maalumu. Ufikapo shuleni jitahidi kusoma kwa bidii ili uiokoe familia yako pamoja na Taifa kwa ujumla.

Nafasi uliyopewa ni mlango wa kuingia katika JAHAZI linalokuelekeza kwenye BANDARI ya mafanikio katika maisha.Inabidi uitumie nafasi hii kwa uangalifu ukiweka juhudi zako zote katika maelekezo utakayopewa hapa shuleni,iwe ndani ya darasa au nje.NIDHAMU, UTIIna USHIKIRIANO ni mambo muhimu yatakayo kuwezesha kufikia mafanikio haya.Unatazamiwa kutafuta MAARIFA kukuza TAALUMA,kutunza MAZINGIRA na kuwa MTIIFU.Mwisho napenda kukutakia maandalizi mema ya kujiunga naShule ya Sekondari Makongoro.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

CHENGE J.M
MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI MAKONGORO

FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINA KAMILI LA MWANAFUNZI: _____
2. TAREHE YA KUZALIWA: _____
3. KABILA : _____
4. DINI: _____
5. SHULE ATOKAYO: _____
6. MWANAFUNZI ANATOKA MTAA WA/ KIJIJI CHA _____
7. KATA YA: _____ TARAFA YA: _____
8. WILAYA YA: _____ MKOA WA: _____
9. WAZAZI WOTE WAPO HAI.MMOJA YU-HAI/YATIMA (FUTA ISIYOHUSIKA)
10. JINA KAMILI MZAZI/MLEZI: _____
11. KAZI YA MZAZI/MLEZI: _____ KAMA MLEZI TAJA UHUSIANO _____
12. ANUANI YA MZAZI/MLEZI:_____SIMU: _____

(a) Nimekubali nafasi niliyopewa na kuwa nitafuata sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Sheria zote na kanuni za shule nimezisoma na kuzielewa.

(b) Nitahakikisha na ninaahidi kuhudhuria darasani siku zote za masomo.

(c) Nitahakikisha nasoma kwa bidii na maarifa. Sitashiriki katika vurugu za aina yoyote ile pindi nikiwa mwanafunzi hapa Makongoro Sekondari. naahidi nitadumisha nidhamu nzuri hapa shuleni.

(d) Sitakuwa tayari kudhalilisha shule yangu.

(e) Nitakubali kuchukuliwa hatua stahiki endapo nitakapoenda kinyume na sheria za shule.

_____ _____

JINA LA MWANAFUNZI **TAREHE**

FOMU YA AHADI YA MZAZI WA MWANAFUNZI

JINA LA MZAZI/MLEZI: _____

(a) Nimesoma na kuyaelewa maelekezo na sheria za shule ya Sekondari Makongoro aliyopewa mwanangu na ninakubaliana nayo.

(b) Ninakubali nafasi aliyopewa mwanangu.

(c) Nitahakikisha kuwa mwanangu anapata mahitaji yake yote muhimu ya shule.

(d) Nitakuwa bega kwa bega na walimu katika kuhakikisha kuwa mwanangu anafuata sheria na kanuni zilizo shuleni. Nidhamu nzuri ya motto ndiyo mafanikio yake.

(e) Naahidi kuwa mwanangu hatashiriki mgomo, fujo na wala makosa ya jinai kama yeye mwenyewe alivyoahidi. Ikitokea akikiuka hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.

_____ _____

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI **TAREHE**

_____

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

MAKONGORO SEKONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 492,
BUNDA.

19/05/2021

The Medical Officer,
……..
……..
……..

RE: …….. (Full name of student)

Please kindly examine the above, named as to his/her Physical and mental for enrolment as a student, the examination should include the following categories.

1. (a) Eye – sight (b) Hearing (c) Limbs (d) Speech (e) Venereal diseases
   (f) Leprosy (g) Epilepsy
2. Neurosis
3. Pregnancy
4. Other serious diseases

THE HEADMASTER

PART B

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a government Medical Officer)
I have examined the above named person and consider that he/she is physically FIT/UNFIT and mentally FIT/UNFIT or full time of schooling.

1. (a) Eye – sight …….
   (b) Hearing ……...
   (c) Limbs ……..
   (d) Speech …….
   (e) Venereal diseases ……
   (f) Leprosy …….
   (g) Epilepsy …….
2. Neurosis ……
3. Pregnancy ……..
4. Other serious diseases ……...

Date: …… Signature: ……..

Station: …….. Designation: ……..